

**OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

Shule ya Sekondari Geita,
S.L.P 72
GEITA.

Simu ya Ofisi : **+255282520075 (masaa ya kazi tu)**
Mkuu wa Shule: **0755372067/0737331472**
Makamu Mkuu wa Shule: **0767677242/0752309170**
Patron/Matron. **0767355360/0755695250/0753462698**

Tarehe _____

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi _____
S.L.P _____

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI GEITA KIDATO CHA TANO
HALMASHAURI YA MJI GEITA MKOA WA GEITA MWAKA 2021.**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2021/2022 Tahasusi ya _____ Shule ya Sekondari Geita ipo umbali wa Kilometa 1.5 kutoka stendi kuu ya mabasi. Usafiri wa Bodaboda au Taxi kuja shuleni unapatikana kutoka stendi kuu ya mabasi. (kwa bodaboda nauli ni Tsh. 1,000/=).

Muhula wa masomo unaanza tarehe 05/07/2021. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe iliyoelekezwa na **OR-TAMISEMI**, mwisho wa kuripoti ni baada ya wiki mbili kama ilivyoelekezwa.

2. Mambo muhimu ya Kuzingatia

2.1 Sare ya Shule

- a) Sare ya Shule hii ni mashati mawili (02) meupe ya tetroni yenye mikono mirefu.
- b) Suruali mbili (02) rangi ya Khaki No. 1 zenye marinda manne (04) mawili (02) upande wa kulia (02) upande wa kushoto.
- c) Sare ya Michezo bukta rangi ya Bluu ikiwa na T-shirt yenye michirizi myeupe (inapatikana duka la shule). Na raba jozi moja (01) kwa ajili ya michezo.
- d) Viatu vya shule ni vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba nyenye visigino vifupi jozi mbili (02).
- e) Soksi fupi jozi mbili (02) rangi nyeusi.
- f) Mkanda wa kuvalia suruali mweusi wa ngozi jozi mbili (02)
- g) Sweta rangi ya bluu (zinapatikana kwenye duka la shule)
- h) Nguo za kushindia ni T-shirt rangi ya kijivu yenye kora nyeusi (inapatikana kwenye duka la shule)
- i) Tai rangi ya khaki jozi mbili (02) (sawa na rangi ya kitambaa cha suruali.

NB:Shati la Shule litachomekewa muda wote unapovaa sare ya Shule.

